# JICHO LA HAZINA

Msajili Wa Hazina Zanzibar

TOLEO NAMBA 007
SEPTEMBA, 2025

*Mashirika ya umma imara, taifa imara, shiriki katika uchaguzi kwa salama na amani*




# Uhusiano wa Umma na Usimamizi wa Mali za Umma





# Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

# **Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar**

## TEHAMA na Uhusiano











**Ofisi ya Majili wa Hazina inatoa wito kwa kila mdau na mwananchi kutoa mapendekezo, ushauri au lolote lile ambaloanahisi litasaidia kulifanya jarida kufikia lengo lake la kuanzishwa na hatimaye kuchangia katika ukusanyaji, usimamizi na matumizi ya fedha katika taasisi za umma. Kwa kushirikiana na kushauriana ndio tutaweza kufanikiwa kujipatia maendeleo tuliyokusudia na kuwa na Zanzibar tunayoitaka.**

# Yaliyomo


04 HISTORIA YA TEHAMA KATIKA TAASISI ZA SERIKALI

05 UBORESHAJI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA (ZGAMIS):

06 TEHAMA KAMA KICHOCHEO CHA UWAJIBIKAJI SERIKALINI

07 UHUSIANO WA UMMA KAMA MSINGI WA UWAZI NA USHIRIKIANO

08 UHUSIANO NA TAASISI NYINGINE

09 UHUSIANO NA JAMII

11 CEO FORUM ZANZIBAR NA TANZANIA BARA

13 NAFASI YA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR

14 MITANDAO YA KIJAMII (X NA INSTAGRAM)

15 FAIDA ZA INSTAGRAM KWA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR

16 MFUMO WA UONDOAJI MALI (ASSET DISPOSAL SYSTEM)

# Historia ya TEHAMA katika taasisi za Serikali

**1. Neno la Utangulizi**



Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar ilianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha mali na mashirika ya uwekazaji wa umma yanasimamiwa ipasavyo. Dhamira kuu ni kukuza ufanisi wa kiutendaji, kuongeza uwajibikaji na kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za serikali.

Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, imekuwa kiungo muhimu katika kusimamia mashirika ya uwekazaji wa umma na mali za serikali kwa kuhakikisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji. Katika zama hizi za kidijitali, ofisi imejikita pia katika kuimarisha mifumo ya teknolojia, habari na mawasiliano (TEHAMA) ili kuendana na kasi ya maendeleo duniani.

**2. Historia ya TEHAMA katika taasisi za Serikali**

Mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990, taasisi nyingi za serikali Afrika Mashariki, ikiwemo Zanzibar, zilianza kutumia kompyuta kwa ajili ya kuandaa nyaraka na kutunza kumbukumbu. Matumizi haya ya awali yalilenga zaidi mashine za uchapaji (typewriters) na baadaye programu rahisi za kuandikia na kuhesabu (Word Processor na Spreadsheets). Huu ulikuwa mwanzo wa mageuzi ya kidijitali katika sekta ya umma.

Miaka ya 1995–2005, taasisi nyingi za serikali zilianza kuunganisha kompyuta kwa kutumia Local Area Networks (LANs). Hatua hii ilirahisisha ushirikiano wa taarifa ndani ya wizara na idara. Aidha, serikali zilianza kuanzisha tovuti rasmi ili kutoa taarifa kwa wananchi na wadau.

Baada ya mwaka 2005, dhana ya Serikali Mtandao (E-Government) ilianza kutekelezwa. Serikali zilijikita katika: Kuunda mifumo ya ndani ya usimamizi wa rasilimali watu na fedha, Kuanza kutumia barua pepe za kiserikali na mfumo wa mawasiliano wa kidijitali. Kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwa kuwezesha wananchi kupata huduma kwa njia ya mtandao.

Ili kusimamia vizuri sera na usimamizi wa TEHAMA, serikali nyingi zilianzisha mamlaka au idara maalum za TEHAMA, mfano: Zanzibar E-Government Agency (eGAZ) – kwa ajili ya kusimamia na kuratibu mifumo ya TEHAMA serikalini. Mashirika ya ulinzi wa mtandao na viwango vya TEHAMA katika ngazi ya kitaifa. Hii iliwezesha kuwepo na sera za kitaifa za TEHAMA na mipango ya muda mrefu ya kidijitali.

**3. Serikali imepiga hatua kubwa kwa kuanzisha mifumo ya kisasa kama:**

- Mfumo wa Usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali (IFIMS).
- Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Umma.
- Mifumo ya Huduma za Kidijitali kwa Wananchi (mfano: usajili wa biashara, huduma za afya, elimu na malipo ya serikali).

TEHAMA imekuwa chombo kikuu cha kuongeza ufanisi, uwazi, na tija katika utumishi wa umma. Kwa jumla, historia inaonesha safari ya mabadiliko kutoka matumizi ya kompyuta za kawaida hadi mifumo ya

# Uboreshaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mali za umma (ZGAMIS)

serikali mtandao na huduma za kidijitali kwa wananchi.

**4. Uboreshaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mali za umma (ZGAMIS):**

Mfumo huu wa kidijitali unarahisisha ukusanyaji wa taarifa, usimamizi wa mali na uandaaji wa ripoti kwa wakati. Mfumo umefanyiwa marekebisho makubwa kutoka ule wa zamani kufikia huu wa sasa. Umeongezwa moduli kama vile Uthibitisho (Verification), (Adjustment) na Matengenezo (Maintanance), pamoja na kufanya maboresho makubwa ya moduli zilizokuwepo awali kama vile Dashbodi, Usajili wa mali (asset register), uhamishaji wa mali (Asset Transfer), Uondoaji wa mali (Asset Disposal) na Ripoti.

**5.TEHAMA katika Usimamizi wa Mali za Umma na Mashirika ya uwekazaji wa umma, Zanzibar**

Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, ni chombo cha serikali chenye dhamana ya kuhakikisha mali za umma na mashirika ya uwekezaji wa umma yanasimamiwa kwa uwazi, ufanisi na uwajibikaji. Katika kutekeleza jukumu hili, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imekuwa injini kuu ya mageuzi, ikileta mbinu za kidijitali zinazorahisisha ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na utoaji wa taarifa.

**6. TEHAMA kama nyenzo ya msingi**

TEHAMA inatoa mfumo thabiti unaorahisisha utendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar. Kupitia mifumo ya kidijitali, ofisi inaweza:

●Kuhifadhi na kufuatilia taarifa za mali za serikali.

●Kusimamia mashirika ya uwekazaji wa umma kwa kutumia takwimu sahihi.

●Kurahisisha utoaji wa ripoti kwa serikali na wadau wengine.

Mfano wa utekelezaji ni mfumo wa **ZGAMIS (Zanzibar Government Assets and Management Information System)** unaowezesha usimamizi wa mali za umma kwa njia ya kisasa.

**7. TEHAMA na Usimamizi wa Mali za Umma**

Mali za umma zinajumuisha majengo ya serikali, mitambo, ardhi, magari na rasilimali nyinginezo. Changamoto kubwa ni kuhakikisha mali hizi zinatumika ipasavyo, hazipotei, na zinachangia maendeleo ya taifa.

●Kupitia TEHAMA, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inahifadhi daftari la mali za umma kwa njia ya kidijitali.

●Inafanya kufuatilia (tracking) mali kupitia namba za usajili na barcodes.

●TEHAMA pia inaruhusu kufanya ukaguzi wa mara kwa mara (audit) kwa urahisi na kutoa taarifa sahihi za thamani na matumizi ya mali.

●Hii inaongeza uwazi na uwajibikaji, kwani kila mali inaweza kufuatiliwa na kuthibitishwa.

**8. TEHAMA na Usimamizi wa Mashirika ya uwekazaji wa umma**

**Mashirika ya uwekazaji wa umma ni injini ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, changamoto mara nyingi ni:**

●Kutokuwa na taarifa za wakati juu ya utendaji wa



# TEHAMA kama kichocheo cha uwajibikaji serikalini

mashirika.

●Changamoto za mawasiliano kati ya serikali na mashirika.

●Ugumu katika uandaaji wa ripoti sahihi na kwa wakati.

●Kwa kutumia TEHAMA:

●Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar hupokea taarifa za kifedha na kiutendaji kutoka mashirika ya uwekazaji wa umma kupitia mifumo ya kidijitali.

●Huweza kufanya uchambuzi wa takwimu kwa kutumia zana kama Excel ili kubaini mashirika yenye ufanisi na yasiyo na tija.

●Mawasiliano kati ya serikali na mashirika yanaimarishwa kupitia mifumo ya taarifa ya pamoja.

Hii inarahisisha serikali kuchukua hatua mapema (early intervention) pale mashirika yanapokumbwa na changamoto.

**9. TEHAMA kama kichocheo cha uwajibikaji serikalini**

TEHAMA imekuwa injini ya mageuzi katika sekta ya umma. Kupitia mifumo ya kidijitali, serikali inapata uwezo wa kufuatilia mwenendo wa kifedha, kudhibiti matumizi yasiyo sahihi na kuongeza uwazi. Kwa Zanzibar, hii ni hatua kubwa kuelekea uwajibikaji wa juu zaidi katika usimamizi wa mali za umma.

**10. Matokeo kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar**

●Uwajibikaji wa juu zaidi.

●Uwazi katika matumizi ya rasilimali.


●Uamuzi bora wa kisera na kimkakati.

**Hitimisho**

Katika Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, TEHAMA si chombo cha hiari bali ni nguzo ya msingi. Inaiwezesha ofisi kusimamia kwa ufanisi mali za umma na mashirika ya uwekazaji wa umma kwa uwazi, kuongeza uwajibikaji na kuhakikisha rasilimali za taifa zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.



# Uhusiano wa Umma kama msingi wa uwazi na ushirikiano



**Sehemu ya Uhusiano**

**Uhusiano wa Umma katika Usimamizi wa Mali na Mashirika ya uwekazaji wa umma**

Katika kutekeleza majukumu yake kama taasisi ya Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, inao wajibu mkubwa wa kuwa karibu na jamii ili kuhakikisha uwazi, uwajibikaji, na ufanisi wa kazi zake. Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inatumia Uhusiano wa umma (Public Relations – PR) kama chombo muhimu cha mawasiliano kati ya ofisi, serikali na taasisi zake, na wananchi. Uhusiano wa umma ni kiungo kinachowezesha taarifa sahihi, uwazi, na ushirikiano wa kila upande.

**1. Uhusiano wa Umma kama msingi wa uwazi na ushirikiano**

●Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, inatumia Uhusiano wa umma kuwasiliana na mashirika ya uwekazaji wa umma na wananchi ili kutoa na kupokea taarifa sahihi kuhusu mali za umma na utendaji wa mashirika.

●Kupitia uhusiano wa umma, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeweza kuimarisha

●Mashirikiano kati ya ofisi na wadau

● Ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake

●Kutoa na kupokea taarifa sahihi za mashirika ya uwekazaji wa umma, taasisi za umma na jamii, na

●Mashirika ya uwekazaji wa umma na taasisi za umma kuelewa majukumu yao kikamilifu.

●Uhusiano wa umma pia umerahisisha mchakato wa maoni na mrejesho kutoka kwa wananchi na mashirika, ili kuboresha utendaji wa ofisi.

**2. Uhusiano wa Umma na Usimamizi wa Mali za Umma**

Mali za umma zinahitaji uangalizi makini ili kuepuka upotevu, matumizi mabaya, au ubadhirifu. Kupitia uhusiano wa umma:

●Wananchi na taasisi za umma wanapewa taarifa juu ya hali, matumizi, na mipango ya mali za umma. Hii huongeza uwazi, kwani kila mali inafuatiliwa na kuthibitishwa.

●Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar hupokea mrejesho kutoka kwa wadau juu ya matumizi ya mali za umma, jambo linalosaidia kuboresha usimamizi na kupunguza mianya ya udanganyifu.

**3. Uhusiano wa Umma na Usimamizi wa Mashirika ya uwekazaji wa umma**

Mashirika ya uwekazaji wa umma yanahitaji mwongozo na usimamizi thabiti. Uhusiano wa

# Uhusiano na Taasisi Nyingine



umma unasaidia Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar:

- Kufahamisha mashirika kuhusu sera, miongozo na taratibu zinazohusiana na utendaji na fedha.
- Kutenga njia za mawasiliano ya mara kwa mara, ili mashirika ya uwekazaji wa umma yasikose taarifa muhimu zinazohitaji utekelezaji.
- Kutengeneza ripoti na mrejesho kwa mashirika yanayokidhi au kushindwa kufikia malengo, na hivyo kuboresha utendaji kwa usahihi.



**4. Uhusiano na Taasisi Nyingine**

Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, imejenga mahusiano ya karibu na taasisi za kitaifa na kimataifa ili kubadilishana uzoefu, kujifunza mbinu mpya za usimamizi, kurahisisha utendaji wa kazi wenye tija na matokeo, na kuimarisha mifumo ya kifedha na kiteknolojia na masuala mengine ya kiuongozi. Kwa taasisi za ndani tunashirikiana na ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania, IDoT, eGaz, ZICTIA na kwa upande wa kimataifa tumeshirikiana na UN.

Katika kuendeleza mashirikiano na tasisi mbalimbali maafisa wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, Bwana Mustafa Omar Abdalla Kibe, Mkuu wa kitengo cha huduma za sheria na Bi Ahlam Abdalla Azzan, Afisa kutoka Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji, walishiriki mkutano wa wakuu wa taasisi (CEOS

# Uhusiano na Jamii







FORUM 2025) na wenyeviti wa bodi uliofanyika tarehe 23-26/2025 Jijini Arusha, ulioandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania. Mkutano ambao ulijadili mada mbalimbali kama vile, Mageuzi na Utendaji (Bw. Nehemiah Mchechu), Rasilimali Watu na AI (Dkt. Lufunyo Hussein), Kutoka Urasimu Hadi Uwepesi (Bi. Fatma M. Abdallah), ESG – Mazingira, Jamii na Utawala (Dkt. Neema Kiure) na nyingi nyenginezo.


**5. Uhusiano na Jamii**

Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inatambua nafasi yake kama kiungo kati ya serikali, mashirika ya uwekazaji wa umma na wananchi. Kupitia TEHAMA, wananchi sasa wanaweza kupata taarifa kwa urahisi zaidi kupitia tovuti ya ofisi, mitandao ya kijamii na machapisho rasmi.

Vilevile, tunashirikiana na wadau mbalimbali katika tafiti na machapisho ya kitaalamu juu ya shughuli zinazofanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, kwa madhumini ya kuboresha kazi na kuondoa changamoto zinazoibuliwa na tafiti na machapisho ya kitaalam. Mfano halisi ni utafiti uliofanywa na Simai Silima Juma & Dr. Fatuma Simba Ikuja, 2023, wenye Kichwa cha habari (title) kifuatacho:

***"Identifying Key Challenges in Public Asset Management: A Case Study on Traceability and Monitoring Inefficiencies in Zanzibar's Public Institutions"*** (Simai Silima Juma & Dr. Fatuma Simba Ikuja, 2023).

Kwa mujibu wa tafiti ya kisayansi (Simai & Ikuja, 2025), changamoto za usimamizi wa mali za umma Zanzibar zimejikita katika udhaifu wa mifumo ya ufuatiliaji, ukosefu wa kitengo maalum cha usimamizi wa mali, na upungufu/ ukosefu wa mafunzo ya kitaalamu.



IRJMETS

e-ISSN: 2582-5208

International Research Journal of Modernization in Engineering Technology and Science

( Peer-Reviewed, Open Access, Fully Refereed International Journal )

Volume:07/Issue:07/July-2025 Impact Factor- 8.187 www.irjmets.com

**IDENTIFYING KEY CHALLENGES IN PUBLIC ASSET MANAGEMENT: A CASE STUDY ON TRACEABILITY AND MONITORING INEFFICIENCIES IN ZANZIBAR'S PUBLIC INSTITUTIONS**

**Simai Silima Juma (Kirosa)*1, Dr. Fatuma Simba Ikuja*2**

*1,2Department Of Computer Science And Engineering (CSE), College Of Information And Communication Technologies (Coict), University Of Dar Es Salaam, P.O. Box 33335, Dar Es Salaam, Tanzania.

DOI: https://www.doi.org/10.56726/IRJMETS80827

**ABSTRACT**

This study explored major challenges in public asset management in Zanzibar, with a focus on traceability and monitoring within government institutions. Adopting a qualitative case study approach underpinned by Public Sector Accountability Theory, the research followed a descriptive framework and gathered data through interviews, document reviews, and direct field observations. Fifty participants were purposefully selected, including department heads, asset management officers, and finance staff. The interview process was validated through expert input and pilot testing, while data credibility was maintained using triangulation and ethical protocols. Thematic analysis guided the interpretation of data, presented in narrative form. The findings pointed to significant barriers such as the absence of standardized monitoring procedures, limited use of digital tracking systems, and insufficient staff capacity. These weaknesses were associated with poor accountability, inefficient resource management, and weak service delivery. The study concluded that effective asset traceability and monitoring require policy changes, digital system implementation, and institutional capacity development. It recommended that the Government of Zanzibar adopt integrated digital asset management tools and reinforce institutional frameworks to improve transparency, accountability, and the efficient use of public assets.

**Keywords:** Public Asset Management, Traceability, Monitoring, Accountability, Institutional Efficiency, Zanzibar.

**I. INTRODUCTION**

Proper management of public assets plays a vital role in achieving transparent governance and ensuring long-

Utafiti huu umeisaida sana Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, katika kuboresha utendaji kazi na kuondoa changamoto zilizoibuliwa, kwani umekuja na suluhisho za changamoto hizo, kama kuanzishwa kwa kitengo maalum kwa kila taasisi, ufuatiliaji wa msimbo, visasisho vya simu, ujumuishaji wa API (barcode tracking, mobile updates, API integration), mafunzo kwa watumishi wote, na kurekebisha sera za serikali ili kuhakikisha ufuatiliaji na uwajibikaji. Hii ni moja ya faida ya uhusiano mzuri na wadau mbalimbali.

**Hitimisho:**

Uhusiano wa umma ni kiungo cha msingi kinachounganisha Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, mali za umma, na mashirika ya uwekazaji wa umma. Kupitia Uhusiano wa umma, ofisi inapata uwezo wa kusimamia mali na mashirika kwa uwazi na ushirikiano, kuhakikisha uwajibikaji na kufanya maamuzi ya kisera na kimkakati kwa msingi wa taarifa sahihi.

## Picha na Matukio

Sehemu hii inajumuisha picha za mikutano, mafunzo, na shughuli mbalimbali.







Kupitia jitihada za kuimarisha mifumo ya Uhusiano na TEHAMA, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inaendelea kuwa chachu ya uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika usimamizi wa mali za umma KWA kutoa mafunzo kwa watumishi.








ZANZIBAR CEOs FORUM

MSAJILI WA HAZINA
OMH
THE TREASURY REGISTRAR OF ZANZIBAR





# CEO Forum Zanzibar na Tanzania Bara






**Utangulizi**

Mashirika ya umma yamekuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Tanzania Bara na Zanzibar

CEO Forum ni jukwaa la viongozi waandamizi wa mashirika ya umma na sekta binafsi kujadili changamoto, fursa, na mustakabali wa mashirika ya umma

Mwaka 2025, mikutano ya CEO Forum Zanzibar (Golden Tulip, 11-13 Mei, 2025) na Tanzania Bara (Arusha, 23-26, Agosti 2025) imeleta dira mpya ya mageuzi ya mashirika ya umma, mageuzi ya sera, na kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

**CEO Forum Zanzibar 2025**

Kauli mbiu ni "Uongozi Bunifu na Mashirikiano kwa Maendeleo Endelevu"

**Mada kuu zilizojadiliwa:**

1. Uongozi bunifu na Mashirikiano katika kufikia maendeleo endelevu ulimwenguni na Zanzibar
2. Kuimarisha mashirika ya uwekezaji wa umma kupitia Uongozi na Ushirikiano.
3. Uongozi na Utawala kwa mashirika ya uwekezaji wa umma
4. Ubia baina ya Taasisi za Umma na Taasisi binafsi;
5. Michango ya sekta binafsi na sekta za Umma katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi
6. Ulazima wa Taasisi Binafsi na Taasisi za Uwekezaji wa Umma kufuata utaratibu wa ki Mazingira, Jamii na Utawala Bora;
7. Mikakati mbadala ya kupata fedha kwa ajili ya kuendesha miradi;
8. Jinsi ya Wakuu wa Taasisi wanavyoweza kusimamia ufanisi katika ukaguzi wa ndani;
9. Ufuatiliaji na Tathmini;
10. Uwezo wa kutambua na kudhibiti hisia kwa viongozi;
11. Mabadiliko ya Kidijitali katika Mashirika ya Umma;
12. Sera katika maeneo ya kazi na uwajibikaji kisheria;
13. Kuimarisha Taasisi za umma dhidi ya ubadhirifu

**Maazimio ya Zanzibar (8):**

- Kuimarisha uongozi na utawala bora katika mashirika ya umma.
- Kukuza ubunifu na ubora wa huduma kwa wananchi.
- Kutambua na kudhibiti vihatarishi vya mashirika.
- Kutangaza na kufuatilia matukio kupitia ESG.
- Kusimamia na kuharakisha mabadiliko ya kidijitali.
- Kufanya CEO Forum Zanzibar kuwa endelevu na ya kila mwaka.
- Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi.
- Kuanzisha Kamati ya Ufuatiliaji chini ya Ofisi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar

# Nafasi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar

kwa utekelezaji wa maazimio.

**CEO Forum Tanzania Bara 2025**

Kauli mbiu **"Ushirikiano Endelevu kwa Ushindani wa Kimataifa"**

**Mada kuu zilizojadiliwa:**

●Mageuzi ya mashirika ya umma (SOEs reforms)

●Nafasi ya teknolojia mpya (AI, blockchain, data)

●Uwajibikaji wa kifedha na utawala bora

●Uendelezaji wa ESG (Environment, Social and Governance)

●Ubunifu na ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi

**Maazimio ya Tanzania Bara (9):**

i. Kuimarisha usimamizi wa rasilimali na kuongeza ufanisi

ii. Harmonization ya matumizi ya TEHAMA ili kuongeza ubunifu

iii. Mashirika ya umma kuoanisha shughuli na Dira ya Maendeleo 2050

iv. Mapitio ya sera na sheria za mashirika ya umma

v. TRO (Bara) kuendeleza vigezo vya kutambua mashirika bora

vi. Kuendeleza maamuzi yanayozingatia tafiti (research-based decisions)

vii. Kupunguza utegemezi wa bajeti kuu

viii. Kuimarisha utekelezaji wa ESG kuanzia mwaka wa fedha 2025/26

ix. Kubadilisha jina la mkutano kuwa C-CEOs Forum kuanzia mwaka 2026/27

**Nafasi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar**

Ulinganisho wa maazimio ya Zanzibar na Tanzania Bara unaonesha mfanano katika maeneo ya uwajibikaji, TEHAMA, ESG na ushirikiano wa sekta binafsi. Zanzibar imejikita zaidi katika uongozi bunifu na ufuatiliaji wa karibu chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, huku Bara ikijikita kwenye mageuzi ya sera na ushindani wa kimataifa.

**Hitimisho**

CEO Forum Tanzania Bara na Zanzibar yamejidhihirisha kama majukwaa muhimu ya kuimarisha usimamizi wa mashirika ya umma na kuchochea mshikamano wa kitaifa. Kwa Zanzibar, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, utekelezaji wa maazimio haya unatoa fursa ya kujenga mashirika yenye uwajibikaji, ubunifu, na mchango mkubwa katika uchumi wa taifa. CEO Forum ni daraja la kuunganisha serikali, mashirika ya umma, sekta binafsi, na wananchi katika safari ya kujenga uchumi shirikishi na endelevu.



# Mitandao ya Kijamii (X na Instagram)

**Tovuti Rasmi (Website)**

Katika zama hizi za kidijitali, tovuti rasmi ya taasisi ni zaidi ya jukwaa la kusambaza taarifa; ni kitovu cha mawasiliano, uwazi na uwajibikaji. Tovuti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar (www.trosmz.go.tz) imejengwa mahsusi kwa ajili ya kuwa lango kuu la upatikanaji wa taarifa na nyaraka muhimu zinazohusiana na usimamizi wa mashirika na mali za umma.

**Misingi ya Tovuti**

1. Kitovu cha Taarifa Rasmi: Tovuti hii ni chanzo cha taarifa sahihi na za kuaminika kuhusu sera, sheria, na miongozo inayosimamia mashirika ya umma na usimamizi wa mali za serikali.


2. Hifadhi ya Nyaraka na Ripoti: Nyaraka muhimu, ikiwa ni pamoja na ripoti za kifedha, taarifa za mikutano, maazimio, na miongozo ya kiutendaji, zinapatikana kwa urahisi kupitia tovuti. Hii inarahisisha upatikanaji wa taarifa kwa taasisi, wadau wa maendeleo, na wananchi.

3. Uwazi na Uwajibikaji: Kwa kuweka taarifa wazi mtandaoni, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inaonyesha dhamira yake ya kuongeza uwazi wa kiutendaji na kuimarisha uwajibikaji wa mashirika ya umma. Hii pia hupunguza utegemezi wa mawasiliano ya karatasi na kuongeza ufanisi wa utendaji.

**Faida kwa TROSMZ na Jamii**

●Kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar: hupunguza mzigo wa maombi ya taarifa kwa barua kwa kuwa wadau hupata taarifa moja kwa moja mtandaoni.

●Kwa Mashirika na Taasisi za Umma: kupata mwongozo wa haraka kupitia nyaraka na miongozo iliyohifadhiwa kwenye tovuti.




●Kwa Wananchi: huongeza imani kwa serikali kwa kuwa taarifa muhimu zinapatikana kwa uwazi bila vikwazo.

●Kwa Wadau wa Maendeleo na Wawekezaji: tovuti inarahisisha utafutaji wa taarifa zinazohusiana na sera, fursa za ubia (PPP), na mwenendo wa mashirika ya umma.

Kwa ujumla, tovuti ya www.trosmz.go.tz siyo tu chombo cha teknolojia, bali ni jukwaa la kitaifa la mawasiliano na uwazi. Kupitia tovuti hii, tunawapatia wananchi na wadau nyenzo ya kuaminika ya kupata taarifa, na kwa kufanya hivyo inaimarisha uwajibikaji, ushirikiano, na ufanisi katika usimamizi wa mashirika na mali za umma Zanzibar.

**Mitandao ya Kijamii (X na Instagram)**

Katika zama za mawasiliano ya kidijitali, X (zamani Twitter) imekuwa jukwaa la haraka zaidi la kusambaza taarifa na kushirikiana na wadau. Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeanzisha ukurasa rasmi wa X kwa anuani @trosmz_zanzibar, ambao ni sehemu muhimu ya mkakati wake wa mawasiliano na uhusiano wa umma.

Majukumu ya Akaunti ya X (@trosmz_zanzibar)

1. Kusambaza Taarifa za Haraka: Akaunti hii hutumika kutangaza mara moja maamuzi ya kitaasisi, taarifa za mikutano, na mabadiliko muhimu yanayohusu mashirika ya umma.

2. Tangazo za Kitaasisi: Kupitia X, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar hutangaza ratiba za mikutano, taarifa za maazimio, pamoja na maelezo kuhusu huduma na mifumo mipya kama vile ZGAMIS.

3. Mawasiliano na Wadau: Wadadisi, watafiti, na wananchi wanaweza kufuatilia taarifa moja kwa moja, na wakati mwingine kushiriki mijadala kwa njia ya majibu (replies) au kusambaza ujumbe (retweets).

●Faida za Kutumia X kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar

Uharaka: taarifa zinafika mara moja kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya Zanzibar.

●Uwazi: kwa kutoa taarifa za mara kwa mara, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar huongeza imani na uaminifu wa wananchi na wadau.

●Ushirikishwaji: X ni jukwaa linalowafikia wadau wengi, wakiwemo vijana, wawekezaji, na mashirika ya kimataifa.

●Ufuatiliaji wa Hisia za Jamii: kupitia majibu na mrejesho

# Faida za Instagram kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar

(feedback), Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inaweza kubaini maoni ya wananchi kuhusu mashirika ya umma na sera zinazotekelezwa.

Akaunti ya @trosmz_zanzibar siyo tu chombo cha matangazo, bali ni njia ya kujenga daraja kati ya serikali na wananchi. Kupitia X, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inaimarisha uwazi, ushirikiano, na mshikamano wa kitaifa kwa kuhakikisha kila mdau anapata taarifa sahihi kwa wakati.

**Instagram: @tro_zanzibar**

Instagram imekuwa moja ya mitandao ya kijamii yenye ushawishi mkubwa duniani, hususan kwa vijana na makundi ya kijamii yanayopenda mawasiliano ya picha na video. Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar hutumia ukurasa wake rasmi wa Instagram kwa anuani @tro_zanzibar kama jukwaa la kushirikiana kwa karibu na wananchi na wadau mbalimbali.






**Majukumu ya Akaunti ya Instagram (@tro_zanzibar)**

1. Kuwasilisha Ujumbe kwa Ubunifu:
Kupitia machapisho yenye ubunifu wa kimaudhui na kiona (visual storytelling), Ofisi huwasilisha ujumbe kwa namna inayoeleweka kirahisi kwa wananchi, hasa vijana.

2. Kukuza Ushirikiano na Wananchi:
Instagram hurahisisha Ofisi kusikia mrejesho wa moja kwa moja kupitia maoni (comments) na "likes", na hivyo kuongeza mshirikiano wa kijamii.

3. Kuhamasisha Uwazi na Uwajibikaji:
Kwa kushirikisha taarifa za moja kwa moja za shughuli zake, Ofisi hujijengea taswira ya uwazi na ya taasisi inayowajibika kwa wananchi.

**Faida za Instagram kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar**

- Kufikia Vijana kwa Ufanisi: vijana wengi hutumia Instagram, hivyo akaunti hii ni jukwaa bora la kueneza taarifa muhimu za serikali.

- Kukuza Uaminifu: picha na video halisi hufanya wananchi waone shughuli za Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kwa uwazi.

- Kujenga Jamii Shirikishi: Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar huimarisha mshikamano na kuunganisha wananchi kupitia mawasiliano ya moja kwa moja.

- Kuweka Historia ya Kiona (Visual Archive): akaunti inahifadhi kumbukumbu za shughuli muhimu ambazo zinabaki kama rejea ya kihistoria.

Akaunti ya @tro_zanzibar siyo tu jukwaa la kijamii, bali ni nguzo ya uwazi, mshirikiano, na uwajibikaji kati ya Ofisi na wananchi wake. Kupitia Instagram, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar huimarisha uhusiano na jamii, kuunganisha vijana, na kuonyesha kwa uwazi namna inavyotekeleza majukumu yake ya kusimamia mashirika na mali za umma.


**Mfumo wa Usajili wa Mali (ZGAMIS)**

Zanzibar Government Assets Management Information System (ZGAMIS) ni mfumo wa kidijitali ulioandaliwa mahsusi kusimamia mali zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mfumo huu ni kiini cha mageuzi katika usimamizi wa mali za umma kwani umeondoa changamoto nyingi zilizokuwepo awali katika ukusanyaji, uhifadhi, na ufuatiliaji wa taarifa za mali za serikali

Awali, mfumo huu ulikuwa na uwezo mdogo wa kimsingi, lakini kupitia marekebisho makubwa yaliyofanywa hivi karibuni, ZGAMIS umeboreshwa na kuongezewa moduli mpya zenye manufaa makubwa kwa usimamizi wa mali. Miongoni mwa moduli hizo mpya ni:

- Uthibitisho (Verification): kuhakikisha taarifa za mali zilizohifadhiwa kwenye mfumo zinawiana na uhalisia uliopo katika taasisi husika.

# Mfumo wa Uondoaji Mali (Asset Disposal System)




●Marekebisho (Adjustment): kuruhusu kufanya marekebisho ya taarifa pale panapohitajika bila kupoteza rekodi za awali, jambo linaloongeza uwazi na ufuatiliaji wa kihistoria.

●Matengenezo (Maintenance): kuweka kumbukumbu za ukarabati na huduma za mali, hivyo kusaidia kuongeza muda wa matumizi na kupunguza gharama za uondoaji mapema.

Aidha, moduli zilizokuwepo awali zimefanyiwa maboresho makubwa ili kuongeza ufanisi na urahisi wa matumizi. Hizi ni pamoja na:

●Dashbodi (Dashboard): yenye muonekano wa kisasa na taarifa za haraka kwa watumishi na wakuu wa taasisi kuhusu mali walizonazo.

●Usajili wa Mali (Asset Register): kurahisisha mchakato wa kusajili mali mpya kwa urahisi na kwa usahihi mkubwa.

●Uhamishaji wa Mali (Asset Transfer): kuwezesha uhamisho wa mali kati ya taasisi kwa uwazi na bila urasimu usio wa lazima.

●Uondoaji wa Mali (Asset Disposal): kurahisisha hatua ya kuondoa mali zilizopitwa na wakati au zisizotumika tena kwa mujibu wa taratibu.

●Ripoti (Reports): kutoa taarifa sahihi na zinazochambuliwa vizuri kwa ajili ya matumizi ya kiutawala na kisera.

### Faida Kuu za ZGAMIS

Maboresho haya yameufanya mfumo wa ZGAMIS kuwa chombo cha kuaminika na cha kisasa kinachowezesha:

Ufuatiliaji na Uwajibikaji (Traceability & Accountability): kila mali ya serikali inaweza kufuatiliwa kutoka hatua ya ununuzi, matumizi, matengenezo, hadi uondoaji wake.

Kupunguza Upotevu na Matumizi Mabaya: mfumo unafunga mianya ya udanganyifu, ubadhirifu, na matumizi holela ya mali za umma.


Utoaji wa Ripoti Sahihi: Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar taasisi zingine za serikali hupata ripoti kwa wakati ili kusaidia maamuzi ya kiutendaji na kisera.

Kwa ujumla, ZGAMIS si tu mfumo wa kiufundi, bali ni nguzo ya uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa mali za umma Zanzibar. Kupitia mfumo huu, serikali inaimarisha imani ya wananchi na wadau, huku ikihakikisha rasilimali za taifa zinatunzwa na kutumika ipasavyo kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

### Mfumo wa Uondoaji Mali (Asset Disposal System)

Katika mzunguko wa maisha ya mali za umma, hatua ya mwisho mara nyingi imekuwa chanzo cha changamoto kubwa za uwazi na udhibiti. Ili kutatua tatizo hili, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeanzisha Mfumo wa Uondoaji Mali (Asset Disposal System), mfumo wa kisasa wa kidijitali unaolenga kudhibiti, kufuatilia, na kurahisisha mchakato wa kuondoa mali za umma.

Mfumo huu ni sehemu muhimu ya mageuzi ya kiutawala kwa sababu unashughulika na mali zilizopitwa na wakati, zisizotumika, au zile ambazo gharama za kuzihifadhi ni kubwa kuliko manufaa yake.



# Misingi na Faida za Mfumo huu

**Misingi na Faida za Mfumo huu**

1. Kufuata Taratibu za Kisheria:
Mfumo unahakikisha kuwa kila hatua ya kuondoa mali inafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni, na miongozo ya serikali. Hii inazuia mianya ya matumizi mabaya na kulinda maslahi ya taifa.

2. Uwajibikaji na Uwazi:
Kupitia mfumo huu, taarifa zote kuhusu mali zinazotarajiwa kuondolewa hutunzwa na kushirikishwa kwa uwazi. Hii ni pamoja na taarifa za thamani, hali ya mali, na mbinu iliyotumika kuiondoa (kama mnada, kuuzwa, au kuharibiwa).


3. Kujenga Ushindani wa Haki:
Kwa kuwa taarifa za mali zinazouzwa au kuondolewa zinatolewa kwa uwazi, wadau wote (wananchi, wafanyabiashara, na taasisi binafsi) hupata nafasi sawa ya kushiriki katika mchakato wa ununuzi. Hii huongeza imani ya umma na kupunguza hatari ya upendeleo au ubadhirifu.


**Mchango katika Utawala Bora**

**Mfumo wa Uondoaji Mali unachangia moja kwa moja katika kuongeza:**

- Ufanisi wa kifedha: mali zisizotumika hazihifadhiwi kwa gharama zisizo na tija.
- Uwajibikaji wa taasisi: kila hatua ya kuondoa mali inaweza kufuatiliwa kwa urahisi.
- Uwazi wa kijamii: wananchi na wadau wanaoona mchakato wa wazi wanajenga imani kwa taasisi za serikali.

Mfumo huu ni nguzo ya uwajibikaji na uwazi katika hatua ya mwisho ya



# Mfumo wa Usimamizi wa Mashirika ya Umma (OTRMIS)







mzunguko wa maisha ya mali za umma. Kupitia Asset Disposal System, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kuwa mali za serikali zinadhibitiwa ipasavyo kuanzia usajili, matumizi, matengenezo, hadi hatua ya kuondolewa. Hii siyo tu hatua ya kiutawala, bali pia ni mfano wa utekelezaji wa sera ya good governance inayolenga kulinda rasilimali za taifa kwa manufaa ya wananchi wote.

**Mfumo wa Usimamizi wa Mashirika ya Umma (OTRMIS)**

Kwa kuzingatia umuhimu wa mashirika ya umma katika kukuza uchumi wa Zanzibar, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeanzisha mfumo



# Faida za OTRMIS kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar Taifa




wa kidijitali uitwao OTRMIS. Mfumo huu umebuniwa kama nyenzo ya kimkakati inayosaidia kufuatilia, kutathmini, na kusimamia utendaji wa mashirika ya umma kwa uwazi na ufanisi.




**Malengo Makuu ya OTRMIS**

1. Kuwezesha Ufuatiliaji wa Utendaji:
Mfumo huu unakusanya taarifa za kifedha na kiutendaji za mashirika ya umma kwa wakati halisi (real time). Hii inatoa nafasi kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kuona mwenendo wa mapato, matumizi, na matokeo ya mashirika husika, na kuchukua hatua mapema pale panapobainika changamoto.

2. Uzalishaji wa Takwimu na Ripoti:
Kupitia OTRMIS, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar hupokea ripoti za mara kwa mara kutoka mashirika yote yaliyo chini yake. Ripoti hizi hubeba takwimu za kifedha, taarifa za miradi, na viashiria vya tija, hivyo kusaidia serikali na watunga sera kufanya maamuzi sahihi na yenye ushahidi (evidence-based decisions).

3. Kulinganisha Mashirika kwa Vigezo vya Uwajibikaji na Tija:
OTRMIS hurahisisha kulinganisha mashirika kwa kutumia vigezo vilivyowekwa, kama vile faida, kiwango cha huduma kwa wananchi, uwajibikaji wa kifedha, na ufanisi wa kiutendaji. Hii inasaidia kutambua mashirika bora na kutoa motisha kwa mengine kuboresha utendaji.

4. Kuhusishwa katika CEO Forums na Mikutano ya Tathmini:
Mfumo huu ni nyenzo muhimu kwa maandalizi ya CEO Forums na mikutano mingine ya tathmini ya mashirika ya umma. Takwimu zinazopatikana kupitia OTRMIS hutumika kama msingi wa mijadala, tathmini ya changamoto, na kupanga mikakati mipya ya kuboresha mashirika.

**Faida za OTRMIS kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar Taifa**

●Kuongeza Uwajibikaji: kila shirika linawajibika kuwasilisha taarifa zake kwa wakati na kwa uwazi.

●Kuchochea Ushindani Chanya: kulinganisha mashirika kunaleta hamasa ya kuboresha huduma na kuongeza tija.

●Kutoa Uwazi kwa Serikali na Umma: taarifa zinapokusanywa na kuchambuliwa, zinasaidia kuongeza imani ya wananchi na wadau wa maendeleo.

●Kuimarisha Ufanisi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar: kwa kuwa na mfumo wa kidijitali, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar hupunguza utegemezi wa taarifa za karatasi na urasimu mrefu, hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji wake.

OTRMIS si tu mfumo wa taarifa, bali ni chombo cha kimkakati cha mageuzi ya usimamizi wa mashirika ya umma. Kupitia mfumo huu, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar inajihakikishia uwezo wa kufuatilia mashirika kwa karibu, kupima mchango wao katika uchumi wa taifa, na kutoa mwongozo wa kuboresha utendaji wao. Ni wazi kuwa OTRMIS ni nguzo muhimu katika kujenga mashirika ya umma yenye tija, uwajibikaji, na mchango mkubwa katika dira ya maendeleo ya Zanzibar.

**Hitimisho la TEHAMA**

Kwa kutumia Website, X, Instagram, ZGAMIS, Asset Disposal System, na OTRMIS, TROSMZ inajijengea msingi imara wa kidijitali. Mifumo hii hufanya usimamizi wa mali na mashirika ya umma kuwa wa kisasa, shirikishi, na uwazi, sambamba na dira ya Zanzibar kuelekea maendeleo endelevu.

# JICHO LA HAZINA

TOLEO NAMBA 007
SEPTEMBA, 2025



Msajili Wa Hazina Zanzibar https://trosmz.go.tz/ info@trosmz.go.tz

**MASHIRIKA YA UMMA IMARA, TAIFA IMARA, SHIRIKI KATIKA UCHAGUZI KWA SALAMA NA AMANI**